
Module 1

# KISWAHILI

## Hatua II

## Kutumia Sarufi ya Kiswahili






Institute of Adult Education
Alternative Secondary Education Pathway

# KISWAHILI

## HATUA YA PILI

# Kutumia Sarufi ya Kiswahili

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala

# Hakimiliki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya kazi hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, isipokuwa kwa kunukuu matini fupifupi zinazoweza kutumika kwa ajili ya utafiti na mapitio ya maandiko.

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2023

**ISBN 978-9976-88-168-4**

S. L. B. 20679,
Dar es Salaam.
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
Tanzania
Simu: +255 22 2150838
Baruapepe: info@iae.ac.tz
Tovuti: www. iae.ac.tz

# Shukurani

Moduli hii ni zao la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) iliyotolewa mwaka 2021 kwa Njia ya Elimu Mbadala (AEP), na inaakisi mtaala wa sasa wa elimu ya sekondari ya 2010 nchini Tanzania, kama ulivyopendekezwa na Taasisi ya Elimu Tanzania.

Moduli hii kwa hakika ni matokeo ya juhudi za pamoja za wataalamu mbalimbali kutoka ndani na nje ya TEWW. Hakika TEWW inatambua kabisa mchango muhimu wa wadau wote kwa kutumia muda wao na rasilimali ili kuhakikisha maandalizi madhubuti ya moduli hii.

IAE inatoa shukrani za dhati kwa watu binafsi waliochangia kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha kazi hii. Wafanyakazi wafuatao kutoka ndani na wadau nje ya TEWW wanastahili kuthaminiwa na kutambuliwa kwa mchango wao wa dhati katika kuandika na kuboresha moduli hii:

| | |
|---|---|
| Baraka S. Kionywaki | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mratibu) |
| Amina M. Abubakar | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mratibu Msaidizi) |
| Tabia Mchakama | Shule ya Sekondari Zanaki (Mpitiaji) |
| Melania Michael | Shule ya Sekondari Mji Mpya (Mpitiaji) |
| Eric Samba | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mhariri) |
| Janeth Mzava | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Katibu Muhtasi) |

...................................................

Dkt. Michael W. Ng'umbi

**Mkurugenzi**

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

# Yaliyomo

**Kuhusu Moduli hii** 1

Muundo wa Moduli ............ 1

**Maelezo ya Jumla kuhusu Moduli** 3

Karibu katika Moduli hii ............ 3
Umahiri wa Jumla ............ 3
Mbinu za Usomaji ............ 3
Je, unahitaji msaada? ............ 4
Mazoezi ............ 4

**Namna ya Kutumia Moduli hii** 5

Ishara za Pambizo ............ 5

**Somo la Kwanza** 6

Kubainisha Njia za Kuongeza Msamiati wa Lugha ............ 6
Utangulizi ............ 6
Matokeo ya kujifunza ............ 6
Muktadha Unaosababisha Kuhitaji Maneno ............ 6
Miktadha Inayosababisha Kuhitajika kwa Maneno Mapya ............ 6
Njia za Uundaji wa Maneno ............ 7
Kutumia Maneno katika Miktadha mbalimbali ............ 9
Tafakuri ............ 10
Zoezi la Nyumbani ............ 10

**Somo la Pili** 11

Kutumia ngeli za Nomino katika Upatanisho wa Kisarufi ............ 11
Utangulizi ............ 11
Matokeo ya kujifunza ............ 11
Dhana ya Ngeli ............ 11
Maana ya Ngeli ............ 11
Misingi ya Upangaji wa Ngeli za Nomino ............ 11
Msingi wa Kisasa ............ 11
Upatanisho wa Kisarufi ............ 12
Misingi ya Mgawanyo wa Ngeli ............ 14
Tafakuri ............ 18
Zoezi la Nyumbani ............ 18

**Somo la Tatu** 19

KufafanuaTungo....19
Utangulizi....19
Matokeo ya kujifunza....19
Dhana, Dhima na Aina za Tungo....19
Tungo Neno....20
Tungo Virai/ Kikundi....20
Virai....20
Aina za Virai....21
Tungo Kishazi....24
Aina za Vishazi....24
Tungo Sentensi....26
Uanishaji wa Sentensi....27
Sehemu kuu za sentensi....30
Kiima (K)....30
Kiarifu....32
Tafakuri....33
Zoezi la Nyumbani....33

**Somo la Nne** 35

Kuchanganua Sentensi....35
Utangulizi....35
Matokeo ya kujifunza....35
Dhana ya uchanganuzi sentensi na hatua zake....35
Kuchanganua sentensi....36
Njia ya jedwali....36
Njia ya matawi....37
Uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia istilahi za kimuundo....38
Njia ya matawi....38
Tafakuri....40
Zoezi la Nyumbani....40

**Faharasa**....**41**
**Marejeleo**....**42**

## Kuhusu Moduli hii

Moduli hii imetayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli zote zilizotayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima zina muundo sawa, kama inavyoelezwa hapa chini.

## Muundo wa Moduli

### Maelezo ya Jumla kuhusu Moduli

Maelezo ya jumla kuhusu moduli hii hutoa utangulizi wa jumla wa moduli. Taarifa zinazopatikana katika maelezo ya jumla kuhusu moduli zitakusaidia kuamua:

- kama moduli hii inakufaa;
- kile unachohitaji kukijua zaidi;
- unachoweza kutarajia kutoka katika moduli;
- muda utakaohitaji ili kukamilisha moduli.

Maelezo haya ya jumla pia hutoa mwongozo juu ya:

- mbinu za usomaji;
- mahali pa kupata msaada;
- mazoezi ya nyumbani na tathmini;
- ishara za vitendo mbalimbali
- masomo.

Tunasisitiza usome maelezo ya jumla kuhusu moduli kwa makini kabla ya kuanza masomo yako.

### Yaliyomo kwenye Moduli.

Moduli hii imegawanywa katika masomo manne. Kila somo lina:

- utangulizi wa yaliyomo kwenye somo;
- matokeo ya somo;
- maudhui ya somo;
- Mazoezi mbalimbali ya somo;
- mazoezi ya nyumbani na/au tathmini, kama inavyohitajika.

### Marejeo

Kwa wale wanaopenda kujifunza mengi zaid juu ya moduli hii, tunawapa orodha ya marejeo ya ziada mwishoni ambayo yanaweza kuwa vitabu, makala au tovuti.

## Maoni yako

Baada ya kukamilisha moduli hii inayohusu Kutumia Sarufi ya Kiswahili, tutashukuru ikiwa utatenga muda mfupi kutoa maoni yako kuhusu kipengele chochote cha moduli hii. Maoni yako yanaweza kuhusu:

- aliyomo kwenye moduli na muundo wake;
- makala za kusoma kwa moduli na marejeo mengine;
- mazoezi ya nyumbani ya moduli;
- tathmini za moduli;
- muda wa moduli;
- usaidizi katika moduli (wahadhiri waliosimamia moduli, usaidizi wa kiufundi, n.k.)

Endapo utatoa maoni mwafaka utatusaidia kuboresha moduli hii.

## Maelezo ya Jumla kuhusu Moduli

### Karibu katika Moduli hii

Ndugu mwanafunzi, moduli hii ni ya kwanza katika hatua hii ya II. Pia ni moduli ya kwanza katika mfululizo wa moduli tatu utakazotakiwa kuzisoma na kujifunza lugha ya Kiswahili. Moduli hii ya kutumia Sarufi ya Kiswahili ina masomo manne. Somo la kwanza ni Kubainisha njia za kuongeza Msamiati, somo la pili ni Kutumia Ngeli za Nomino katika upatanisho wa kisarufi, somo la tatu ni kufafanua tungo na somo la nne linahusu kuchanganua sentensi. Karibu sana katika moduli hii.

### Umahiri wa Jumla

Baada ya kukamilisha moduli ya Kiswahili hatua ya II inayoitwa Kutumia Sarufi ya Kiswahili utaweza:

- kuwasiliana kwa njia zote kwa ufasaha.

### Mbinu za Usomaji

Kwa kuwa wewe ni mwanafunzi wa Elimu Changamani baada ya msingi, utaratibu wako wa kusoma utakuwa tofauti na ule ulioutumia ulipokuwa bado shuleni: utachagua unachotaka kukisoma, utakuwa na motisha ya kitaalamu na/au ya kibinafsi inayokusukuma, na bila shaka utakuwa ukiratibu shughuli zako za kiusomaji huku ukizingatia majukumu yako mengine ya kitaalamu au ya nyumbani.

Kimsingi, utakuwa unayadhibiti mazingira yako ya masomo. Kwa hivyo, utahitajika kufikiria juu ya masuala ya utendaji yanayohusiana na udhibiti wa wakati, kuweka malengo n.k. Pengine utahitaji kujizoesha tena katika maeneo kama uandishi wa insha, namna ya kuimudu mitihani, na kutumia mtandao kama marejeo ya ujifunzaji. Mambo utakayozingatia sana ni *muda* na *nafasi,* yaani muda unaotenga kwa masomo yako na mazingira unamosomea.

Tunapendekeza utumie fursa hii kabla ya kuanza kujisomea, ufahamu anuani chache za tovuti unazoweza kuzitumia kujifunza.

- http://www.how-to-study.com/

Tovuti ya "How to study" yaani "Jinsi ya kujifunza" imetengwa mahsusi kwa ajili ya marejeo ya mbinu za usomaji. Utaelekezwa namna ya kupata maelekezo kuhusu sifa za mahali pa kujisomea, namna ya kuandika kumbukumbu, mikakati ya kusoma vitabu vya kiada na ziada, na kutumia vyanzo mbalimbali vya kumbukumbu.

- http://www.ucc.vt.edu/stdysk/stdyhlp.html

Hii ni tovuti ya Kitengo cha Masuala ya Wanafunzi. Utapata maelekezo kuhusu upangaji wa muda wako, orodha-hakiki ya mbinu za usomaji, mbinu za kumakinika jambo, udhibiti wa mazingira ya kusomea, kuandika kumbukumbu, namna ya kusoma insha kwa kusudi la kuchanganua, na mbinu za kukumbuka.

- http://www.howtostudy.org/resources.php

Hii ni tovuti nyingine ya "jinsi ya kusoma" iliyo na anuani muhimu kuhusu udhibiti wa wakati, kusoma kwa ufanisi, mbinu za kusaili/kusikiliza/kuchunguza, ujifunzaji wa kiutendaji, jinsi ya kujenga kumbukumbu, na vidokezo vya namna ya kudumisha motisha uliyonayo.

Anuani hizo za tovuti hapo juu ni mapendekezo yetu. Ikiwa unataka kupata anuani za tovuti zaidi, zitafute kwa anuani hii ya tovuti www.google.com kisha uandike "self-study basics" (misingi ya usomaji binafsi), "self-study tips" (vidokezo vya usomaji binafsi), "self-study skills" (mbinu za usomi binafsi) au tovuti nyingine zenye mada kama hizo.

## Je, unahitaji msaada?

Ndugu mwanafunzi, katika mchakato wako wa kujifunza, unaweza kuhitaji msaada kuhusu mambo mbalimbali, kwa mfano, mahali unapoweza kupata msaada na namna ya kupata msaada huo. Pamoja na hayo, unaweza kuhitaji ufafanuzi kuhusu moduli unazozisoma. Hivyo basi, unashauriwa kuomba ufafanuzi wa yote hayo kwa mratibu wa kituo chako au mwezeshaji wako. Pia, unaweza kufungua tovuti ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yenye anwani hii: www.iae.ac.tz au piga simu hii +255 22 2150838.

## Mazoezi












Baada ya kila somo, unahitajika kujibu maswali ya zoezi la somo. Majibu ya zoezi la kila somo hutayawasilisha kwa mwezeshaji wako, bali ni kwa ajili ya kufanya tafakuri ya ulichojifunza. Pia, utapewa majaribio na mazoezi ambayo utayafanya na kuyawasilisha kama utakavyoongozwa na mwezeshaji wako. Pamoja na hayo, utatakiwa kufanya mitihani ya majaribio kwa ajili ya upimaji wa maendeleo yako ya kitaaluma.

# Namna ya Kutumia Moduli hii

## Ishara za Pambizo

Huku ukifanya kazi katika Moduli hii, utagundua kwamba kuna matumizi mengi ya ishara za pambizo. Ishara hizi zina jukumu la kuashiria aina fulani ya matini, kazi mpya au kubadilika kwa zoezi. Ishara hizo zimetumiwa ili kukuongoza ujue namna ya kuitumia Moduli hii.

Seti nzima ya ishara imetolewa hapa chini. Tunapendekeza kuwa ujizoeshe ishara hizi na maana yake kabla ya kuanza masomo yako.

| | | | |
|---|---|---|---|
| <br>Zoezi | <br>Tathmini | <br>Zoezi la Nyumbani | <br>Uchunguzi Kifani |
| <br>Mjadala | <br>Zoezi la Kikundi | <br>Usaidizi | <br>Kumbuka! |
| <br>Matokeo | <br>Kusoma | <br>Tafakari | <br>Mbinu za Usomaji |
| <br>Muhtasari | <br>Istilahi | <br>Muda | <br>Kidokezi |

# Somo la Kwanza

## Kubainisha Njia za Kuongeza Msamiati wa Lugha

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, nadhani ulishapata uelewa juu ya sarufi ya lugha na kuelewa maana, miundo na umuhimu wa sarufi ya lugha ya Kiswahili. Rejea katika Somo la Kwanza katika Moduli ya Kwanza ya Hatua ya Kwanza. Sasa karibu katika Somo la Kwanza katika Moduli ya Kwanza ya Hatua ya Pili. Somo hili ni mwendelezo wa Somo la Tatu kutoka katika moduli ya nne, linalohusu uundaji wa maneno kwa kutumia uambishaji na mnyumbuliko. Bila shaka katika moduli hiyo ulijifunza maneno mapya. Naamini umekuwa ukitumia maneno mbalimbali katika mawasiliano yako ya kila siku. Maneno hayo ndio yanaitwa misamiati. Kwa hiyo, karibu ujifunze njia nyingine za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili.

## Matokeo ya kujifunza

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- *Kueleza* mazingira yanayosababisha kuhitaji maneno mapya;
- *Kuunda* maneno kwa kutumia njia mbalimbali; na
- *Kutumia* maneno katika miktadha mbalimbali.

### Muktadha Unaosababisha Kuhitaji Maneno

Ndugu mwanafunzi, jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili imekuwa ikikumbwa na mabadiliko ya kimaendeleo. Maendeleo hayo yamefanya lugha ihitaji maneno ili yaweze kukidhi haja ya matumizi kwa jamii husika. Kutokana na ukweli huo, maneno mapya yanaweza kuibuka kwa lengo la kuziba pengo hilo.

Tembelea katika miktadha mbalimbali kama vile ya kielimu, kiutamaduni, kidini, kiofisi na kibiashara. Unaweza kugundua tofauti gani ya matumizi ya maneno kutoka katika miktadha hiyo? Unafikiri ni kwa nini?

#### Miktadha Inayosababisha Kuhitajika kwa Maneno Mapya

#### Uchumi

Kwa mfano maneno yaliyozuka katika muktadha huu ni kikokotozi, muamala, mrabaha (uhasibu), makinikia (madini), fedha, pesa, shilingi, senti, benki, ushuru, n.k. Maneno haya yametokea katika maendeleo ya kiuchumi ya kutumia fedha badala ya kubadilishana bidhaa.

**Sayansi na Teknolojia**

Maneno yaliyotokea katika muktadha huu ni gari, tovuti (website), king'amuzi (decoda), jokofu (fridge), kangavute (generator), na pangaboi (fan), mtandao, simumtelezo, nukushi, n.k.

**Utamaduni**

Maneno yaliyozuka katika kukuza na kuendeleza utamaduni ni pamoja na gauni, sketi, dansi, bendi, kijiko, uma, mvinyo, hereni na vipuri, shanga, n.k.

**Huduma za jamii**

Maneno yaliyozuka katika huduma mbalimbali za kijamii kama vile afya ni umwari (karantini), plasta, zahanati, hospitali na katika elimu ni darasa, kalamu, daftari, penseli.

**Mabadiliko ya Mfumo wa Siasa na utawala**

Mabadiliko ya mfumo wa siasa na utawala husaidia kukuza msamiati kwa mfano: Tumbua (ondoa madarakani wasiowajibika) ng'atuka (jiudhuru), walalahoi, fisadi, chakachua, vigogo, chama tawala, chama pinzani, dikteta, mapinduzi, n.k.

Jadili kwenye kikundi maswali yafuatayo:

1. Unadhani ingetokea nini endapo usingekuwepo uwezekano wa kuongeza msamiati katika lugha?
2. Utatumia njia gani ili kutaja jina la kitu ambacho wewe ni mara yako ya kwanza kukiona?
3. Pitia mazingira tofauti yanayokuzunguka, chunguza misamiati tofauti tofauti wanayotumia.

## Njia za Uundaji wa Maneno

Baada ya kujifunza umuhimu wa kuongezeka msamiati kulingana na haja ya matumizi kwa wazungumzaji wa jamii fulani. Hebu sasa tujifunze njia hizi za uundaji wa maneno. Zipo njia kadhaa za kuunda maneno. Njia hizo ni:

i) **Kuambatanisha Maneno**

Hii ni njia ya kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kupata neno moja ambalo lina maana tofauti na maneno ya awali.

Mfano:

| | | |
|---|---|---|
| Bata + mzinga | - | Batamzinga |
| Mwana + nchi | - | Mwananchi |
| Mwana + jeshi | - | Mwanajeshi |
| Pembe + tatu | - | Pembetatu |
| Mwana + isimu + jamii | - | Mwanaisimujamii |
| Jungu + kuu | - | Jungukuu |

ii) **Kutohoa Maneno kutoka Lugha nyingine**

Kila lugha ina tabia ya kuchukua maneno kutoka lugha nyingine na kuyabadilisha ili yalingane na mfumo wa lugha husika, kimatamshi na kimaandishi. Tendo hilo la kufanya maneno yafuate kanuni za lugha nyingine huitwa **utohoaji.**

Lugha ya Kiswahili imetohoa maneno kutoka lugha nyingine na kuyabadilisha maneno hayo ili yafuate taratibu za lugha ya Kiswahili kimaandishi na kimatamshi. Maneno yanayotoholewa hulazimika kusanifishwa na vyombo vilivyowekwa kufanya kazi hiyo kabla hayajaruhusiwa kutumika rasmi. Kwa mfano angalia Jedwali 1.1.

**Jedwali 1.1: Utohoaji katika lugha ya Kiswahili**

| **Kiswahili** | **Lugha ya mwanzo** | **Neno** |
|---|---|---|
| Shati | Kiingereza | Shirt |
| Hela | Kidachi | Hella |
| Sigara | Kiingereza | Cigarette |
| Shule | Kijerumani | Schule |
| Shukurani | Kiarabu | Shukran |
| Salamu | Kiarabu | Salaam |
| Ngeli | Kihaya | Engeli |
| Ng'atuka | Kizanaki | Ng'atuka |
| Kitivo | Kisambaa/Kipare | Kitivo |
| Ndafu | Kichaga | Ndafu |
| Duka | Kihindi | Duka |

iii) **Kufananisha Sauti, Umbo na Tabia**

Baadhi ya maneno ya Kiswahili yametokana na kuhusianisha na milio, umbile, tabia au matumizi ya kitu kinachohusika.

kwa mfano:

a) Kufananisha sauti (onomatopoeia au tanakali sauti) kwa njia hii tunapata maneno kama vile pikipiki, nyau, mtutu, malapa, mvumo, cherehani, kuku n.k.
b) Kuangalia umbo au maumbile ya kitu. Njia hii huunda maneno kwa kuangalia muonekano wa kitu kinachopewa jina tunapata maneno kama *kifaru* (gari la kivita la jeshi ambalo linafanana na mnyama anayeitwa kifaru). *Mkono wa tembo* (limetokana na mfanano wa umbo la ndizi na mkonga wa tembo). *Kidole tumbo (*ni sehemu ya utumbo mpana ambalo linafanana na umbile la kidole).

c) Kukipa kifaa jina kutokana na matumizi yake, kwa mfano *kipimajoto, ufagio, kifuniko, kibanio.*

iv) **Urudufishaji**

Urudufishaji ni kitendo cha kurudia sehemu ya neno au neno zima ili kuunda neno lingine. Maana ya neno linaloundwa huwa tofauti na maana ya neno la asili. Kwa mfano:

- Sawa + sawa - Sawasawa
- Pole + pole - Polepole
- Kinyume + nyume - Kinyumenyume
- Kimya + kimya - Kimyakimya
- Kizungu+ zungu - Kizunguzungu
- Bara + bara - Barabara

v) **Kufupisha Maneno**

Ufupishaji huu hufanywa kwa kuchagua baadhi ya silabi kutoka katika baadhi ya maneno ya kikundi au silabi za kila neno katika kikundi ili kupata neno moja. Kwa mfano:

- Taasisi ya Elimu Tanzania – TET
- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI
- Baraza la Kiswahili Tanzania – BAKITA
- Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania – UWAVITA
- Chama Cha Mapinduzi – CCM
- Upungufu wa Kinga Mwilini – UKIMWI
- Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – TATAKI

vi) **Kubadilisha Herufi**

Katika njia hii neno linaweza kuunda maneno mengine zaidi kwa kubadilisha herufi za neno husika.

Kwa mfano;

a) tai – *ita, ati, tia*
b) zoea – *ozea, azoe, aoze*
c) Lima - *mali, imla, lami.*

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza njia mbalimbali za uundaji wa maneno. Sasa karibu tuwe sote katika utumiaji wa maneno katika miktadha mbalimbali.

## Kutumia Maneno katika Miktadha mbalimbali

Matumizi ya maneno hutofautiana kutoka muktadha mmoja na mwingine. Hivyo, matumizi ya maneno hayo yanaweza kuwa sahihi kwa muktadha mwingine.

Kwa mfano neno **sentensi**

Katika muktadha wa kielimu neno hili linatumika kama kifungu cha maneno chenye kuleta maana lakini katika muktadha wa kisheria sentensi inatumika kama adhabu/hukumu.

## Tafakuri

Ndugu mwanafunzi, mpaka hapo umeshajifunza njia muhimu za kuongeza msamiati katika lugha. Katika kujifunza unadhani uelewa ulioupata utaweza kukusaidia katika kuunda misamiati mbalimbali? Ujuzi ulioupata utakusaidiaje katika maisha yako ya kila siku?

## Zoezi la Nyumbani

1. Fafanua njia za uundaji maneno kwa mifano.
2 a) Eleza maana ya muktadha.

b) Eleza maneno mbalimbali yanavyotumika katika miktadha mbalimbali kama vile;

- Afya
- Kwenye basi/ kituo cha daladala
- Sokoni
- Mahakamani

3. Kwa kutumia njia ya kuambatanisha maneno toa mifano mbalimbali ya maneno hayo.
4. Fafanua njia ya kufupisha maneno kwa mifano.

# Somo la Pili

## Kutumia Ngeli za Nomino katika Upatanisho wa Kisarufi

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza somo la kwanza linalohusu njia za kuongeza msamiati katika lugha ya Kiswahili, sasa tujifunze kwa pamoja ngeli za nomino. Kabla ya kujifunza ngeli hizo yafaa tujiulize nini maana ya ngeli? Madhumuni mahususi ya somo hili ni kukuwezesha kupanga majina ya Kiswahili katika ngeli kulingana na vipashio vya upatanishi wa kisarufi kati ya majina hayo na viambishi awali katika vitenzi.

## Matokeo ya Kujifunza

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kueleza dhana ya ngeli za nomino;
- Kubainisha misingi ya upatanishi wa ngeli kimapokea na kisasa; na
- Kufafanua mgawanyo wa ngeli kwa misingi ya upatanishi wa kisarufi.

### Dhana ya Ngeli

Ndugu mwanafunzi, bila shaka umeshawahi kusikia dhana ya ngeli za nomino ikitajwa na wenzako. Kaeni kwenye kikundi kisha mjadili kwa kina dhana hii kabla ya kuendelea kujifunza sehemu inayofuata.

#### Maana ya Ngeli

Ngeli ni neno linalotokana na lugha ya Kihaya, likiwa na maana ya aina au mgawanyo wa kitu au vitu katika makundi. Hivyo, ngeli ni aina au namna ya kuweka majina katika makundi yanayofanana au yanayowiana. Kwa hiyo, ngeli za nomino maana yake ni aina au makundi ya majina au nomino.

### Misingi ya Upangaji wa Ngeli za Nomino

Katika upangaji wa ngeli kuna mitazamo/misingi miwili, nayo ni:

i) Msingi wa kimapokeo.
ii) Msingi wa kisasa.

Katika hatua hii utajifunza msingi mmoja ambao ni msingi wa kisasa.

### Msingi wa Kisasa

Msingi huu hujulikana pia kama msingi wa **upatanisho wa kisarufi**, au **msingi wa mpangilio wa maneno kisarufi, au kisintaksia**.

Huu ni mtazamo unaogawa majina katika ngeli zake kulingana na upatanisho wa kisarufi kati ya jina na viambishi awali vilivyo katika vivumishi na vitenzi. Kwa mujibu wa mtazamo huu, ngeli za majina ya Kiswahili ni tisa. Sasa tutazame kwanza dhana ya upatanisho wa kisarufi.

## Upatanisho wa Kisarufi

Tunajifunza upatanisho wa kisarufi ili tuweze kutoa miundo sahihi ya Kiswahili kwa kutumia utaratibu wa kanuni za sarufi. **Upatanisho wa kisarufi** ni utaratibu wa kuhusiana kwa viambishi awali vya vitenzi na vile vya majina, viwakilishi pia vivumishi vinavyotokea katika sentensi moja.

i) Kwa mfano: Jina na kivumishi

Mtoto mdogo

Sentensi inaelekeza upatanisho wa nomino na kivumishi.

ii) Jina Kivumishi Kitenzi

kisu kikali kimepotea.

Katika sentensi hizo hapa nomino huelekeza upatanisho huo wa kivumishi na kitenzi.

iii) Tuangalie mfano wa sentensi zifuatazo katika umoja na wingi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| A | B |
| 1. Jembe hili limevunjika | Majembe haya yamevunjika. |
| 2. Kopo lile limechakaa | Makopo yale yamechakaa. |

Katika sentensi za kifungu A kiambishi 'li' kimetumika kupatanisha kisarufi nomino, vivumishi na vitenzi. Katika kifungu B kiambishi 'ya' ndicho kinacholeta uwiano wa kisarufi. Sentensi zilizotajwa katika kifungu A na B zinatumia kiambishi 'li' katika umoja na 'ya' katika wingi ili kuleta upatanishi wa kisarufi.

Tujaribu tena kutazama mifano ya sentensi zifuatazo:-

1. Kiziwi yule anaishi hapa.
2. Ugonjwa wa UKIMWI umeenea.
3. Kiti hiki kimevunjika.
4. Mtoto amebanwa na ubao.
5. Wimbo huu unanipa faraja.
6. Kile kitakupendeza zaidi.
7. Kitenge kile kimechanika.
8. Kijana yule ana akili.

Baada ya kuchunguza kwa makini mifano hiyo hapo juu, utagundua kuwa sentensi zote hizo ziko katika hali ya umoja, pia baadhi ya maneno yana upatanishi wa kisarufi wa aina moja. Hebu jaribu kutathimini kwa kina na badili sentensi hizo ziwe katika hali ya wingi, kisha bainisha viambishi vinavyoonesha uwiano wa kisarufi unaofanana. Bila shaka, kwa kufanya hivyo unaweza kupata mafungu ya nomino yenye ufanano ufuatao:

| a | b | c |
|---|---|---|
| Kisu | Mtoto | Ugonjwa |
| Kiti | Kiziwi | |
| Kitenge | Kijana | Wimbo |

Mwainisho huu wa nomino, katika makundi au mafungu kulingana na upatanishi wa kisarufi wa nomino hizo, vivumishi na vitenzi katika sentensi, hutupatia ngeli za nomino.

Ngeli za nomino hutambulishwa na viambishi vya upatanisho wa kisarufi kati ya nomino au viwakilishi vyake, vivumishi na vitenzi katika sentensi. Tuangalie Jedwali 2.2 hadi 2.4:

**Jedwali 2.2: Upatanisho wa kisarufi kwa ngeli ya ki-vi**

**Kifungu A**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Kiti hiki kimevunjika | Viti hivi vimevunjika |
| Kitenge kile kimechanika | Vitenge vile vimechanika |
| Kile kitakupendeza | Vile vitakupendeza |

Jedwali 2.2 linaonesha viambishi vya upatanisho wa kisarufi ambavyo ni Ki katika umoja na Vi katika wingi. Hivyo ngeli za nomino hizo ni ki-vi.

**Jedwali 2.3: Upatanisho wa kisarufi kwa ngeli ya yu-a-wa**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mtoto amebanwa na ubao | Watoto wamebanwa na mbao |
| Mtoto yumo ndani | Watoto wamo ndani |

Jedwali 2.3 linaonesha viambishi vya upatanisho wa kisarufi ambavyo ni yu na a katika umoja na wa katika wingi. Hivyo, ngeli za nomino hizo ni yu–a– wa–.

**Jedwali 2.4: Upatanisho wa kisarufi kwa ngeli ya u - zi**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ule umeanguka juzi | Zile zimeanguka |
| Wimbo huu umenipa faraja | Nyimbo hizi zimenipa faraja |
| Uzi umekatika | Nyuzi zimekatika |

Jedwali 2.4 linaonesha viambishi vya upatanisho wa kisarufi ambavyo ni 'U' katika umoja na 'ZI' katika wingi. Ngeli ya nomino hizo ni U-ZI.

**Zoezi 1**

Ndugu mwanafunzi, hadi sasa umepata maarifa kuhusu ngeli za majina. Hebu jaribu kukaa na wenzako katika kikundi kisha mjadili maswali yafuatayo:

1. Fikiria vitu mbalimbali ambavyo vipo kijijini au mtaani kwenu. Orodhesha majina ya vitu hivyo katika ngeli zinazofaa. Hakikisha jibu lako kwa kuitungia sentensi kila nomino ili kuona kama viambishi vya upatanisho wa kisarufi vinakubaliana na vile vya ngeli hiyo.
2. Kwa mtazamo wa kisasa, ngeli za makundi ya majina zilipangwa kutegemea nini?

## Misingi ya Mgawanyo wa Ngeli

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza upatanisho wa kisarufi, katika Sehemu ya Kwanza, ni vema sasa katika sehemu hii kujifunza jinsi ngeli zilivyogawanywa kwa msingi wa upatanisho wa kisarufi. Ili iwe rahisi kwako kuona mgawanyo huu, chunguza jedwali 2.5, na utafakari mifano zaidi.

**Jedwali 2.5: Aina na mifano ya ngeli za Kiswahili**

| Na. | Aina za ngeli | Viambishi | Umoja/Wingi | Mfano |
|---|---|---|---|---|
| 1. | YU, -A-, WA | YU-<br>A-<br>WA- | Umoja<br><br>Wingi | Mtoto yu mgojwa<br>Mtoto anaumwa<br>Watoto wanaumwa |
| 2. | U – I | U<br><br>I | Umoja<br><br>Wingi | Mpera umekauka<br>Mpodo umechomwa<br>Mipera imekauka<br>Mipodo imechomwa |
| 3. | LI - YA | LI-<br>YA- | Umoja<br><br>Wingi | Ua limenyauka<br>Embe limeoza<br>Maua yamenyauka<br>Maembe yameoza |
| 4. | KI – VI | KI-<br>VI- | Umoja<br><br>Wingi | Kikombe kimevunjika<br>Kisu kimepotea<br>Vikombe vimevunjika<br>Visu vimepotea |
| 5. | I – ZI | I-<br>ZI- | Umoja<br>Wingi | Barabara itatengenezwa<br>Nyumba imebomoka<br>Barabara zitatengenezwa<br>Nyumba zimebomoka |

| Na. | Aina za ngeli | Viambishi | Umoja/Wingi | Mfano |
|---|---|---|---|---|
| 6. | U – ZI | U-<br><br>ZI- | Umoja<br><br>Wingi | Ufunguo umepatikana<br>Uzi umekwisha<br>Funguo zimepatikana<br>Nyuzi zimekwisha |
| 7. | U –YA | U-<br>YA- | Umoja<br><br>Wingi | Uovu umekithiri<br>Ugonjwa umeenea<br>Maovu yamekithiri<br>Magonjwa yameenea |
| 8. | KU | KU | Umoja | Kucheza kunachangamsha<br>Kuimba kwake kunanifurahisha |
| 9. | PA, MU, KU | PA-<br>MU-<br>KU- | | Pahali pale pana maji<br>Mule muna giza<br>Kule kunapendeza |

Kwa msingi wa upatanisho wa kisarufi, nomino za Kiswahili zimegawanyika katika ngeli tisa, kama ilivyooneshwa katika Jedwali 2.5.

Ni dhahiri kuwa ukilichunguza jedwali hilo kwa makini utang'amua viambishi ambavyo vinapatanisha majina hayo au viwakilishi vyake. Kwa kuwa majina ni yaleyale tunayoyatumia kila siku katika shughuli zetu, haitakuwia vigumu kuyagawa majina yaliyomo katika lugha ya Kiswahili katika ngeli. Tuangalie mfano wa ngeli ya kwanza, ambayo ni ya YU- A- WA – Viambishi vyake ni YU- A- katika umoja na WA katika wingi.
Mfano wa sentensi ni kama huu ufuatao:

Umoja: Mama ameingia ndani.
Mtu anatoroka.
Wingi: Akina mama wameingia ndani
Watu wanatoroka

Kama ulivyoona, jambo la kuzingatia katika mfano huo ni kwamba kitambulisho cha ngeli za majina si umbo la jina bali ni viambishi vinavyopatanisha majina hayo na kitenzi au kivumishi.

Sasa hebu tuangalie mfano wa ngeli ya pili ambayo ni ya U-I – viambishi vyake ni U-katika umoja na I- katika wingi mfano wa sentensi ni kama.
Umoja: Mbuyu umeanguka.
Wingi : Mibuyu imeanguka.
Umoja: Mkoba umechakaa.
Wingi : Mikoba imechakaa.

Ndugu mwanafunzi, hadi sasa umejifunza ngeli za nomino na jinsi mgawanyo wake unavyoleta upatanisho wa kisarufi. Upatanisho huo umejitokeza katika nomino (majina), vitenzi na vivumishi katika umoja na wingi.

### Viambishi vya O-rejeshi

Hebu tutazame jinsi kipashio cha ngeli za nomino kinavyoweza kujitokeza kama kiambishi ndani ya kitenzi. Kiambishi ngeli huitwa – O- rejeshi yaani ni kiangama kinachotumiwa katika sentensi kuonesha jambo lililokwishatajwa au linalojulikana kwa mfano angalia sentensi zifuatazo:

- Wanafunzi wali-o-itwa hawakufika.
- Misitu ili-yo-chomwa imeathirika.
- Vipusa vili-vyo-fichwa vimepatikana.

Hapa tunaona kuwa mofimu zilizopigiwa mstari ndizo zinazoonyesha 'O' rejeshi.

Katika urejeshi wa 'O'- tunaona kuwa vitenzi vinabeba kiambishi ngeli VIANGAMA – 'O' isipokuwa kama nomino iliyotajwa ni ngeli ya YU-A-WA umoja, Urejeshi kwa ngeli hiyo hutumia 'e' badala ya 'O'. Kwa mfano:

a) Kijana aliyepita anatisha;
b) Tembo aliyejeruhiwa anasakwa;
c) Mtoto aliyetoroka atapata adhabu.

Ukitazama mifano hiyo na ukiongeza mifano yako utapata dhana halisi tunayoizungumzia.

Jaribu tena kuwa makini katika kulichunguza jedwali hili ili uweze kuona mfano wa –o- rejeshi kulingana na mgawanyo wa ngeli. Unapaswa kutazama safu zote ili uweze kuona aina za ngeli, viambishi vya ngeli hizo na –o- rejeshi inavyojitokeza.

*Jedwali 2.6: Muundo wa -O- rejeshi katika ngeli*

| Na. | Aina za ngeli | Viambashi vya ngeli | Viambishi vya 'O' | Mifano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Yu – A – WA- | YU-<br>A-<br>WA- | -YE –<br>-O- | Msanii aliyeandika kitabu amezawadiwa.<br>Wasanii walioandika vitabu wamezawadiwa. |
| 2 | U –I- | U-<br>I- | -O-<br>-YO- | Mhogo ulionunuliwa haukuiva vizuri.<br>Mihogo iliyonunuliwa haikuiva vizuri. |
| 3 | LI – YA- | LI-<br>YA- | -LO-<br>-YO | Jiwe lililotupwa limevunja kioo.<br>Mawe yaliyotupwa yamevunja kioo. |
| 4 | KI-VI- | KI-<br>VI- | -CHO-<br>-VYO- | Kinu kilichotengenezwa kinapendeza.<br>Vinu vilivyotengenezwa vinapendeza. |
| 5 | I-ZI- | I-<br>ZI- | -YO-<br>-ZO- | Nguo iliyoungua imetupwa.<br>Nguo zilizoungua zimetupwa. |
| 6 | U-ZI- | U-<br>ZI- | -O-<br>-ZO- | Uzi ulioshonea umekatika.<br>Nyuzi ulizoshonea zimekatika. |
| 7 | U-YA- | U-<br>YA- | -O-<br>-YO- | Ugonjwa ulioenea umekwisha.<br>Magonjwa yaliyoenea yamekwisha. |
| 8 | KU- | KU- | -KO- | Kuimba unakokupenda kwanipendeza. |
| 9 | PA-<br>MU-<br>KU- | PA-<br>MU-<br>KU- | -PO-<br>-MO-<br>-KO- | Pale ulipohamia pamependeza<br>Humo tulimokuwa mna baridi<br>Huko unakokwenda sio salama. |

Baada ya kuona tabia ya vitenzi ya kuonyesha urejeshi wa mtenda au mtendwa unaweza kujipima wewe mwenyewe kwa kutunga sentensi nyingi zenye -O- rejeshi ukitumia nomino za ngeli mchanganyiko. Kwa kila sentensi, onyesha kiambishi cha -O- rejeshi.

## Tafakuri

Umejifunza mgawanyo wa ngeli katika mtazamo wa kisasa. Je umepata ugumu wowote katika kujifunza ngeli? Ni maswali gani mengine unaweza kuwa nayo? Iwapo una maswali yoyote unaweza kuwasiliana na wanafunzi wenzako na mwezeshaji.

## Zoezi la Nyumbani

1. Eleza kazi za viambishi vilivyopigiwa mstari katika maneno yafuatayo: <u>Wa</u>napika, <u>Wa</u>nakiuza, <u>Ki</u>lichopotea, Ana<u>ye</u>fundisha na Ali<u>mo</u>ingia.

2. Kwa kutoa mifano eleza misingi ya mgawanyo wa ngeli kwa mtazamo wa kisasa.

3. Nini maana ya ngeli? Panga nomino zifuatazo katika ngeli zake kwa kufuata mtiririko: kuta, kisu, chupa, nyanya, kiziwi na maiti.

4. Taja nomino tano zipatikanazo katika ngeli ya LI – YA, kisha tunga sentensi kwa kila nomino katika umoja na wingi.

# Somo la Tatu

## Kufafanua Tungo

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, baada ya kumaliza somo la pili katika moduli hii ya kwanza, karibu katika somo la tatu linalohusu kufafanua tungo. Kwakuwa tungo huundwa kwa kutumia maneno, Basi maneno yote uyatumiayo ni tungo. Katika somo hili utajifunza dhana na dhima ya tungo, aina za tungo na sifa zake. Aina hizo za tungo ni Virai, Vishazi na Sentensi.

## Matokeo ya Kujifunza

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kueleza dhana, dhima na aina za tungo;
- Kufafanua neno, virai, vishazi na aina za sentensi katika tungo; na
- Kufafanua sehemu kuu za sentensi.

### Dhana, Dhima na Aina za Tungo

Tungo ni neno au mpangilio wa maneno unaotoa taarifa fulani. Taarifa hiyo inaweza kuwa kamili au isiwe kamili. Vilevile tungo huweza kuonyesha wakati, mahali, namna na nani anayehusika na tendo linavyofanyika. Kwa mfano:

Tungo ambayo haikamilishi taarifa, hudai tungo nyingine ili taarifa ikamilike. Tungo inaweza kuwa:

i) neno moja kwa **mfano:** wanacheza
ii) maneno mawili, kwa **mfano:** wanafunzi wanasikiliza
iii) kikundi cha maneno zaidi ya mawili kwa **mfano:** wananchi watafika kesho.

Kabla ya kuendelea na sehemu inayofuata tunga tungo yoyote ile inayotoa taarifa kamili na isiyotoa taarifa kamili.

Hizo zote ni tungo lakini viwango vya kukamilika kwa taarifa zake vinatofautiana. Kwa msingi huo, tungo za Kiswahili zimegawanyika katika makundi yafuatayo:

a) Neno
b) Virai
c) Vishazi
d) Sentensi

Sasa hebu tuangalie makundi hayo ya tungo kwa kuyafafanua moja baada ya jingine.

## Tungo Neno

Neno ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na kuleta maana, kwa mfano, baba, mama, mtoto, mwalimu, paka, jenga, soma, lima, n.k. Neno huweza kuwa nomino, kitenzi, kivumishi na mengineyo.

**Kuna aina mbili za neno**

Neno sahili ambalo hujengwa na mofimu moja na halina viambishi kwa mfano: baba, nje, hewa, maji

Neno changamani ambalo hujegwa na mofimu zaidi ya moja ambazo huambatana na mzizi wa neno. Tazama mifano katika Jedwali 2.7:

**Jedwali 2.7: Tungo neno**

| **Aina ya neno** | **Neno/kwa mfano** | **Mofimu** |
|---|---|---|
| Jina/nomino | • Mwalimu (changamani)<br>baba (sahili) | Mw-alimu<br>Baba |
| Kivumishi | • Safi (sahili) | Safi |
| Kiwakilishi | • Mimi (sahili) | Mimi |
| Kitenzi | • Analima (changamani)<br>• Anaimba | a-na-lim-a<br>a-na-imb-a |
| Kielezi | • Kabisa (sahili) | Kabisa |
| Kiunganishi | • Na (sahili) | Na |
| Kihisishi/kiingizi | • Lo! (shahili) | Lo! |

Kabla ya kuendelea na sehemu inayofuata taja maneno sahili na maneno changamani.

## Tungo Virai/ Kikundi

### Virai

Kirai au kikundi ni kipashio cha kimuundo kinachoundwa na neno zaidi ya moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu. Kwa kawaida, kirai ni kikubwa kuliko neno.

**Kwa mfano:**

- Mnyama mkubwa
- Kwa kisu

Katika kiwango hiki miundo ya tungo huhusisha maneno mawili au zaidi yanayowekwa pamoja katika mpangilio maalumu unaozingatia uhusiano uliopo baina ya neno kuu na maneno mengine.

Sasa shirikiana na wanafunzi wenzako kujadili kwa kutoa mifano zaidi kuhusu virai na aina zake. Pamoja na majibu mazuri mliyoyapata, linganisha majibu hayo na aina zifuatazo za virai.

## Aina za Virai

### Virai Nomino

Kirai nomino ni kirai kinachotawaliwa na nomino au na uhusiano wa nomino na neno au mafungu ya maneno. Kirai nomino huundwa na maneno yafuatayo kama yalivyopigiwa mistari;

- **Nomino peke yake**

Kwa mfano:
- Adili ni rafiki yangu.
- Nyumba kubwa.

- **Nomino mbili au zaidi zinazounganishwa**

Kwa mfano:
- Mwalimu na wanafunzi wanaandika.
- Kuku na bata wanakula chakula.
- Milima na mabonde inaipamba nchi.

- **Nomino na kivumishi**

Kwa mfano:
- Miti mirefu imeanguka.
- Mtoto yule ni mpole.
- Wanafunzi wetu wanaimba.

- **Kiwakilishi peke yake**

Kwa mfano:
- Wewe unaumwa kichwa.
- Sisi hatujamaliza.
- Wote watasafiri.

- **Kiwakilishi na kivumishi**

Kwa mfano:

- Vyetu vyote vimepotea.
- Yule mwerevu anapendwa sana.
- Kile ambacho kilipotea kimeonekana.

- **Nomino na kishazi tegemezi kivumishi**

Kwa mfano:

- Mtoto aliyekuja jana ameondoka.
- Mbwa aliyepata kichaa ameuawa.

- **Kitenzi jina au kitenzi jina na kivumishi**

Kwa mfano:

- Kuimba kunafurahisha.
- Kusoma kwake ni kwa mashaka.

Baada ya kupitia virai nomino sasa tuangalie aina nyingine ya virai ambavyo ni virai vitenzi.

### Kirai kitenzi (KT)

Kirai kitenzi ni kirai ambacho kinamilikiwa na kitenzi kimoja au zaidi. Kirai kitenzi huweza kujengwa na:

- **Kitenzi kimoja peke yake (T)**

Kwa mfano:

- Wanafunzi wanacheza.
- Mtoto anasoma.
- Mwalimu anafundisha.

- **Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (Ts + T)**

Kwa mfano:

- Mtoto alikuwa anacheza.
  Ts T

- Mama alikuwa anataka kukimbia.
  Ts Ts T

- **Kitenzi, jina na kielezi (T + N + E)**

Kwa mfano:

- Anacheza mpira uwanjani.
  T N E
- Anaimba nyimbo vizuri.
  T N E

- **Kitenzi kishirikishi (t)**

Kwa mfano:

- Ndiye kiongozi.
  t

- Huyu ni mgonjwa.
  t

Maneno yaliyopigiwa mstari katika mifano ya hapo juu ni virai vitenzi Ndugu mwanafunzi, sasa tuone aina nyingine ya virai.

**Kirai kivumishi (KV)**

Kirai kivumishi ni kile ambacho muundo wake umemilikiwa na kivumishi. Kwa kawaida muundo huu huwa ni wa kivumishi na neno au fungu la maneno linaloandamana na vivumishi. Virai vivumishi hujibainisha zaidi kimuundo kama sehemu ya virai nomino, navyo hujengwa kwa vipashio vifuatavyo:

Kwa mfano:

- Watoto kumi wamechaguliwa.
- Maembe yote yameharibika.
- Gari lililoibiwa jana limekamatwa.
- Banda la kuku limejengwa.
- Jengo kubwa limejengwa.
- Shule yetu ina madarasa mengi.

Maneno yaliyopigiwa mstari katika mifano hapo juu ni virai vivumishi. Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza kirai kivumishi, hebu sasa tujifunze aina nyingine ya virai ambayo ni kirai kielezi.

### Kirai kielezi (KE)

Hivi hudokeza namna au jinsi ya utendekaji wa jambo. Aidha hudokeza mahali na wakati lilipotendeka jambo hilo. Kirai kielezi huweza kuundwa kwa kielezi kimoja au zaidi.
Kwa mfano:

- Mvua ilinyesha usiku kucha.
- Tulitembea haraka haraka.
- Mwalimu atarudi baadaye.
- Wanafunzi wanacheza uwanjani.
- Anakuja mara kwa mara.
- Alibisha hodi mara tatu.

Maneno yaliyopigiwa mstari katika mifano hiyo hapo juu ni virai vielezi. Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza aina za virai hebu sasa tuangalie mada ndogo ya vishazi.

## Tungo Kishazi

Ni tungo ya ngazi ya juu kuliko kirai na ya chini kuliko sentensi. Kishazi kinaweza kuwa na muundo wa kiima na kiarifu unaoleta maana kamili au isiyo kamili kutegemeana na kitenzi kilichomo katika kishazi hicho. Kitenzi ni kipashio cha msingi katika kishazi.

### Aina za Vishazi

Kitenzi katika kishazi kinaweza kujitosheleza, yaani kuwa na maana kamili au kutojitosheleza na kutegemea kitenzi cha kishazi kingine ili kukamilisha maana. Kwa msingi huo tunaweza kupata aina mbili za vishazi ambazo ni;

i) Vishazi huru.
ii) Vishazi tegemezi.

### Vishazi huru (α)

Ni kishazi kinachojitosheleza kimaana na kusimama peke yake kama sentensi. Vishazi huru hutambulishwa kwa alama *KHr* au $\alpha$
Kwa mfano:

- Asha anasoma kitabu chake.
- Wanakijiji wamepanda miti shambani kwao.
- Anamkimbilia mtoto wake.

Tungo zilizopo hapo juu ni mifano ya vishazi huru.

**Miundo ya kishazi huru**

a) Kitenzi kikuu peke yake

Kwa mfano;

- Alisoma
- Tunaandika
- Wamejibizana
- Nitaondoka.

b) Nomino, kitenzi kikuu na nomino

Kwa mfano;

- Mwanafunzi anaandika nukuu.
- Mtoto anacheza mpira.

c) Nomino na kitenzi kikuu

Kwa mfano;

- Baba analima.
- Mto umefurika.

d) Nomino kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu

Kwa mfano;

- Mgonjwa atakuwa amelala.
- Mwalimu alikuwa anafundisha.

**Vishazi tegemezi: (β)**

Hiki ni kishazi ambacho hakiwezi kutoa taarifa kamili mpaka kikamilishwe na kishazi huru. Kwa hiyo kishazi tegemezi huacha maswali kwa msomaji kwa kutokukamilika kwake.

Kwa mfano:

- Misitu iliyochomwa.
- Magari waliyokopeshwa.
- Ugonjwa ulioenea.

Maneno yaliyopigiwa mstari ni vishazi tegemezi.

Hivyo tunaweza kuona kuwa vishazi tegemezi peke yake havina uwezo wa kukamilisha taarifa. Vinahitaji kishazi kingine ili kukamilisha ujumbe uliokusudiwa na msemaji. Kiambishi cha -O- rejeshi kilichomo katika kitenzi hubainisha kishazi tegemezi. Vishazi tegemezi vilivyotolewa hapo juu vinadai vishazi vingine (huru) ili kukamilisha ujumbe.

- Misitu iliyochomwa haipendezi.
  (β) (α)
- Magari waliyokopeshwa yameharibika.
  (β) (α)
- Ugonjwa ulioenea utatudhuru.
  (β) (α)

Baada ya dhana ya vishazi kufahamika, jaribu kutambua vishazi mbalimbali katika tungo zifuatazo:

a) Bwana Chapakazi anatayarisha shamba.
b) Kila mara tunafagia viwanja.
c) Kitoweo alichotarajia kimeharibika.
d) Mkaa mlionunua hauwaki.

Kimpangilio, sentensi huundwa na vishazi, hivyo kimuundo vishazi ni vikubwa kuliko virai na vidogo kuliko sentensi. Tazama mpangilio huu.

| |
|---|
| Neno kirai → kishazi → sentensi |

Baada ya kujifunza na kutambua aina za tungo sasa tunga sentensi iliyojengwa na neno kirai na kishazi, kabla ya kuanza kujifunza aina za sentensi.

## Tungo Sentensi

Sentensi ni ngazi ya juu kabisa ya tungo. Ni tungo yenye kutoa taarifa kamili kuhusu jambo fulani. Au sentensi ni kifungu cha maneno kuanzia neno moja na kuendelea chenye kiima na kiarifu chenye kuleta maana kamili.
Kwa mfano:

- Mvua za vuli zimenyesha sana mwaka huu.
- Barabara zimetengenezwa vizuri.
- Jogoo huwika alfajiri.
- Najua kesho utakuja.

Sentensi hizo zinatoa ujumbe uliokamilika. Katika mawasiliano ya kawaida wazungumzaji hutumia sentensi nyingi ili kukamilisha mazungumzo. Pia, wazungumzaji hutumia tungo za aina mbalimbali.

### Uanishaji wa Sentensi

Hapa tutazungumzia uainisho wa sentensi kwa msingi wa muundo. Kabla ya kuendelea tuangalie vifupisho vitakavyotumika katika mada yetu hii.

| | | |
|---|---|---|
| S | = | Sentensi |
| S. S | = | Sentensi sahili |
| S. Amb | = | Sentensi ambatani |
| S.Sh. | = | Sentensi Shurutia |
| S. Ch | = | Sentensi Changamani |

Kama tulivyokwishaona, sentensi ni ngazi ya juu kabisa ya tungo. Bila shaka, unakumbuka kuwa ngazi ya chini ni neno ikifuatiwa na virai, vishazi na ndipo tunapata sentensi.

Kwa hiyo, kazi iliyobaki kwetu ni kuzifanyia kazi sentensi ambazo tunazitumia kila siku katika maisha yetu. Tutazichambua ili tuweze kujua kazi za kila neno katika sentensi, tukishaifanya kazi hiyo tutazipanga na kuziainisha sentensi hizo.

Tuangalie vifupisho vitakavyotusaidia katika uchanganuzi wa sentensi.

| | | |
|---|---|---|
| K | - | Kiima |
| A | - | Kiarifu |
| KT | - | Kikundi tenzi |
| KN | - | Kikundi nomino |
| KE | - | Kikundi kielezi |
| Sh | - | Shamirisho |
| Ch | - | Chagizo |
| Ø | - | Kapa |
| T | - | Kitenzi kikuu |
| Ts | - | Kitenzi kisaidizi |
| t | - | kitenzi kishirikishi |
| $\beta v$ | - | Kishazi tegemezi kivumishi |
| $\alpha$ | - | Kishazi huru |
| $\beta$ | - | Kishazi tegemezi |

### Uanishaji wa Sentensi

Baada ya kuona mifano ya sentensi pamoja na vifupisho vitakavyotumika katika uainishaji wa sentensi sasa tuangalie aina za sentensi.

Kwa kuzingatia muundo wa sentensi tunaweza kubaini kuwa kuna aina nne za sentensi. Aina hizo ni:

a) Sentensi Sahili.
b) Sentensi Changamani.
c) Sentensi Ambatano
d) Sentensi Shurutia.

### Sentensi sahili

Hii ni sentensi ya kishazi huru, kishazi hicho kinaweza kuwa na kifungu tenzi kimoja. Kifungu tenzi hicho kinaweza kuwa kitenzi kikuu, au kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu au kitenzi kishirikishi.

**Kwa kwa mfano:**

- Amelala.
- Mtoto analia sana.
- Tutakuwa tumeondoka.
- Mtoto alikuwa analia.
- Huyu ni mkulima.

### Sentensi changamano/ changamani

Baada ya kuona sentensi sahili, karibu tena tujifunze jinsi sentensi changamani inavyojengwa. Hii inajengwa kwa kutumia kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Tujaribu kuchunguza na kuangalia kwa makini mifano ifuatayo:

i) Nitamweleza atakapofika.
$\alpha$ $\beta$

ii) Nilishtuka aliponieleza mkasa alioupata.
$\alpha$ $\beta$ $\beta$

Kitu cha muhimu katika sentensi hii ni kuwepo kwa kishazi zaidi ya kimoja. Sasa tujaribu kutazama miundo ya sentensi changamano:

a) Kishazi huru kimoja na kishazi tegemenzi kimoja, kwa mfano:

i) Wezi waliosalia watakamatwa.

Sentensi hii ina kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja
- Wezi waliosalia – hiki ni kishazi tegemezi.
- Watakamatwa – hiki ni kishazi huru.

ii) Upepo umeangusha miti iliyokauka.
- Upepo umeangusha miti. hiki ni kishazi huru
- Iliyokauka – ni kishazi tegemezi.

iii) Mtoto aliyeadhibiwa amegeuka na kuwa mtu bora.
- Mtoto aliyeadhibiwa - ni kishazi tegemezi
- Amegeuka na kuwa mtu bora – ni kishazi huru

iv) Shehena iliyosubiriwa imewasili.

- Shehena iliyosubiriwa – ni kishazi tegemezi
- Imewasili – ni kishazi huru

b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (Ts + T) kwa mfano:

- Takataka zilikuwa zimezagaa ukumbini.

  Ts T

- Tunafikiri tutamkuta.

  Ts T

c) Kitenzi kishirikishi

Kwa mfano:

- Huyu ndiye mwenyekiti.

  t

- Mvua ilikuwa haba sana.

  t

- Hawa ndio watoto wetu.

  t

Baada ya kumaliza kujifunza vijenzi vya sentensi changamani sasa bainisha vishazi huru na tegemezi katika sentensi zifuatazo:

1. Watu walioshiriki kulima matuta watafaidika.
2. Ndege iliyopotea tangu juzi haijaonekana.
3. Wanyama wanaovutia wameisha mbugani.

**Sentensi ambatano, (S.Amb)**

i) Hizi zinaweza kujengwa na sentensi mbili au zaidi. Dhana ya uunganishi hutumika kuunga sentensi moja na nyingine kwa mfano zaweza kuwa. S. S + S. S, S.ch + S.ch + S.S. + S.ch.

Kwa mfano:

- Mtoto ameadhibiwa lakini bado anaiba.
- Walitoka darasani wakajipanga kisha wakaenda bwaloni.
- Maria alilima na akapanda.

Maneno yaliyopigiwa mstari ndiyo hutumika kuunga sentensi zilizotolewa mifano hapo juu.

Muundo huu ni sawa na kuunga sentensi sahili mbili au zaidi. Nadhani hizi sentensi si ngeni kwako kwani mifano ya sentensi kama hizi umekutana nayo mara nyingi.

ii) Vile vile sentensi ambatani hujengwa na sentensi changamani moja na kishazi huru kimoja au zaidi.

Kwa mfano:

Kijana aliyefika jana amekwenda msituni lakini kaka yake
S.ch U α

anasoma kitabu.

iii) Sentensi changamano mbili au zaidi.

Kwa mfano:

Mtoto aliyefika jana ameondoka na dada yake aliyeumia
S.ch U S.ch
amelazwa hospitalini.

Inakupasa kukumbuka kuwa sentensi ambatani hutokana na matumizi ya viunganishi na, lakini, tena, ingawa, ijapokuwa n.k.

### Sentensi shurutia (S.sh)

Sentensi hizi hutumika wakati mtu anapotoa masharti. Hii ni sentensi yenye vishazi tegemezi viwili ambavyo utegemezi wake hutokana na mofimu nge, ngali, ngeli na ki ya masharti. Masharti hayo huonesha kwamba ili tukio la pili litokee, sharti tukio la kwanza likamilike.

Sentensi shurutia zenye viangama ngeli, ngali, nge daima huwa katika wakati uliopita.

Hivi ni kusema ikiwa kishazi kimoja kina 'nge' ni lazima cha pili kiwe na 'nge' kwa kwa mfano:

- Angewahi kuingia tungefunga mlango.
- Akija nitafurahi.
- Wangalitoa taarifa wangalimkuta.

## Sehemu kuu za sentensi

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza aina za sentensi. Sasa itakubidi utazame muundo huu wa sentensi kwa undani ili uweze kuchanganua sentensi. Sentensi ina sehemu kuu mbili, nazo ni **kiima na kiarifu**. Muundo huo ndio mjengo wa sentensi yoyote ya kawaida. Unaweza kutafuta mifano mingi zaidi ili ikuwie rahisi kufanya mazoezi. Hebu tuanze na kiima.

### Kiima (K)

Ni sehemu ya sentensi inayotaja nomino (jina) inayohusika na mtenda na mtendwa. Nomino, hiyo inaweza kutajwa bayana au isitajwe kwa kuwa tayari inajulikana kutokana na mazungumzo ya awali. Jina hilo pia huweza kudokezwa katika kitenzi cha sentensi hiyo kwa njia ya kiambishi awali. Hebu tuchunguze vipashio hivi vinavyounda kiima.

Kiima huundwa na:

i) **Nomino moja au zaidi**

- Jongo/analima shamba.
  K
- Wakubwa na wadogo/wataingia.
  K

ii) **Nomino na vivumishi**

- Barabara hii/haipitiki.
  K
- Watoto wadogo/wanakuja.
  K

iii) **Kiwakilishi**

- Hilo /limevunjika.
  K
- Ule/umekatwa matawi.
  K

iv) **Kiwakilishi na kivumishi**

- Wote hawa/wamechoma mkaa.
  K
- Ule mrefu/mmeupata.
  K

v) **Nomino na kishazi tegemezi:**

- Magunia yaliyofichwa/yameuzwa.
  K
- Mti uliopandwa/umestawi.
  K

vi) **Kitenzi Jina**

- Kusoma/kuna manufaa.
  K
- Kuimba/kunafurahisha.
  K

vii) **Kiima kapa**

- Ø /Atakuja kesho.
- Ø /Hatutamuona tena.

Tukumbuke kuwa alama 'K' inaonyesha kuwa sehemu hiyo ya sentensi ni kiima.

**Kiarifu**

Hii ni sehemu ya pili ya sentensi ambayo hutoa taarifa ya jambo linalofanywa na kiima au linalokitokea kiima.

Vipashio vinavyounda kiarifu ni kikundi kitenzi, shamirisho na chagizo. Tutafafanua maana ya hivi vipashio ili uweze kuvielewa na kuvifanyia kazi.

a) **Kikundi tenzi (KT)**

Nafasi hii hukaliwa na maneno yote ya jamii ya vitenzi.

Kwa mfano:

- Kitenzi kikuu kimoja

Ninaondoka.
T

Wanacheza.
T

- Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu

Alikuwa anakuja.
Ts T

Walikuwa wameondoka.
Ts T

- Kitenzi kishirikishi

Hii ndio nzuri.
t

Ndiye ninayemtafuta.
t

b) **Shamirisho (Sh)**

Kitenzi na kikundi nomino (Kt + Kn). Ni kikundi nomino cha kiarifu ambacho hutaja nomino inayotambulisha mtendewa, mtendwa, kitendea au sababu.

Kwa mfano:

- Baba anaandika barua.
  Sh
- Juma amepigiwa ujeuri.
  Sh

Hivyo, majina yaliyojitokeza katika kiarifu kwa mfano barua, ujeuri ni nomino katika kiarifu na hujulikana pia kama shamirisho.

c) **Chagizo (Ch)**

Ni nafasi inayokaliwa na vielezi vyote katika sentensi. Vielezi hivyo vinaweza kuwa vya idadi, namna, wakati au mahali kitendo kilipofanyika. Chagizo pia inaweza kuwa kikundi kielezi kwa mfano,

- Mama alirudi jana usiku.
  Ch

Ili kuweza kupata mwanga zaidi inabidi tuangalie mifano hii hapa pamoja na kutafuta mifano ya ziada itakayosaidia kutambua chagizo katika sentensi.

Kwa mfano:

- Mtoto/alilima shamba lile kwa bidii.
  Ch
- Wawindaji/wamekamatwa Serengeti leo.
  Ch

Kwa hiyo ukumbuke kwamba kikundi kielezi ni kipashio muhimu sana katika kiarifu kwani hueleza zaidi namna tendo (kitenzi) lilivyotokea.

## Tafakuri

Ndugu mwanafunzi, nafikiri umepiga hatua katika juhudi zako za kujifunza Kiswahili. Je, sasa unaweza kueleza maana ya tungo, dhima na aina zake? Je, umeweza kufafanua aina za tungo? Je, mjadala wa utangulizi kuhusu sehemu za sentensi umekupa maarifa ya kutosha kuhusu sehemu za tungo hiyo? Kipi kinakutatiza? Je, somo hili lina maana kwa maisha yako?

## Zoezi la Nyumbani

Baada ya kujifunza sehemu hii ya kiima na kiarifu jibu maswali yafuatayo:

i) Kwa kutumia mifano fafanua vipashio vinavyounda shamirisho na chagizo.

ii) Fafanua dhima ya:

(a) Kiima.

(b) Kiarifu.

iii) Eleza muundo wa sentensi sahili.

1. Chunguza sentensi zifuatazo kisha uoneshe kiima na kiarifu kwa kuweka alama **K** (kiima) na alama **A** (kiarifu)

   i) Maria anapika ugali.
   ii) Askari wote wamerudi vitani.
   iii) Ng'ombe aliyevunjika mguu amepotea.
   iv) Mbuzi aliyenunuliwa jana ameuzwa leo.
   v) Mama na dada wataondoka mchana.

2. Kwa kutumia mifano bainisha sentensi za Kiswahili.

# Somo la Nne

## Kuchanganua Sentensi

### Utangulizi

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza kwa kina aina na miundo ya sentensi Sahili, Ambatani, Changamani na Shurutia sasa unakaribishwa uwe pamoja nami kuchangia mawazo, hoja na mapendekezo yako katika uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia taratibu mbalimbali. Tutaanza kueleza dhana ya uchanganuzi wa sentensi, hatua za uchanganuzi wa sentensi kisha tutachambua pamoja sentensi kwa kutumia njia ya jedwali na njia ya matawi/ngoe.

## Matokeo ya Kujifunza

Mwanafunzi amalizapo somo hili ataweza;

- Kueleza dhana ya uchanganuzi wa sentensi na hatua zake; na
- Kuchanganua sentensi kwa njia ya jedwali na njia ya matawi/ngoe

### Dhana ya uchanganuzi sentensi na hatua zake

Uchanganuzi wa sentensi ni kufafanua vipengele vinavyojenga sentensi katika viwango mbalimbali. Kila sentensi huweza kuchanganuliwa na kubainishwa vipashio vinavyoijenga.

a) Uchanganuzi wa sentensi kimapokeo hufuata hatua zifuatazo:
   i) Kutambua aina ya sentensi inayoshughulikiwa yaani kama ni sentensi ambatani, sahili, changamani.
   ii) Kutambua sehemu kuu za sentensi yaani kiima na kiarifu
   iii) Kutambua vipashio vinavyounda Kiima na Kiarifu vya sentensi hiyo kama vile Kifungu Kitenzi (FT), Shamirisho (SH), na Chagizo (CH).
   iv) Kutambua aina za maneno yanayoijenga sentensi hiyo, kama vile nomino, viwakilishi, vivumishi, vielezi, viunganishi n.k.
   v) Kuandika upya sentensi hiyo.

b) Uchanganuzi wa sentensi kimuundo hufuata hatua zifuatazo:
   i) Kutambua aina ya sentensi inayoshughulikiwa yaani kama ni sentensi ambatani, sahili, changamani.
   ii) Kutambua sehemu kuu za sentensi yaani kiima na kiarifu
   iii) Kutambua vikundi au virai vya sentensi hiyo kama vile kikundi nomino (KN), kikundi tenzi (KT) na kielezi (KE).

iv) Kutambua aina za maneno yanayoijenga sentensi hiyo, kama vile nomino, viwakilishi, vivumishi, vielezi, viunganishi n.k.
v) Kuandika upya sentensi hiyo.

## Kuchanganua sentensi

Kuna njia mbalimbali za uchanganuzi wa sentensi njia hizo ni njia ya maelezo, njia ya jedwali, njia ya matawi, na njia ya mishale.
Katika hatua hii tutachanganua sentensi kwa kutumia njia mbili ambazo ni *njia ya jedwali* na *njia ya matawi.*

### Njia ya jedwali

Sasa tutajaribu kwa mfano mwingine wa sentensi, ili tuuchanganue kwa njia ya jedwali kuonesha kila kipashio
Kwa mfano:

**Jedwali 4.1: Juma anasoma gazeti.**

| **S. Sahili** | | |
|---|---|---|
| **K** | **A** | |
| **KN** | **KT** | **KN** |
| **N** | **T** | **N** |
| Juma | anasoma | gazeti |

**Jedwali 4.2: Wageni wetu wataondoka kesho usiku.**

| **S. Sahili** | | |
|---|---|---|
| **K** | **A** | |
| **KN** | **KT** | **KE** |
| **N + V** | **T** | **E + E** |
| Wageni wetu | Wataondoka | kesho usiku |

**Zoezi 1**

Ndugu mwanafunzi, baada ya kujifunza uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya jedwali hebu jaribu kuchanganua sentensi hizi kwa kutumia njia hiyo.

1. Mwalimu aliyetunga mtihani amesahihisha vizuri.
2. Alisoma kwa bidii lakini hakufaulu mtihani.


Baada ya kujifunza kuchanganua sentensi kwa njia ya jedwali sasa karibu katika kuchanganua sentensi kwa kutumia njia ya Matawi.

**Njia ya matawi**


Njia hii hutumia vistari kuonesha madaraja ya ufafanuzi ambapo picha ya mwisho huonekana kama matawi ya mti.

Tuangalie uchanganuzi huo kwa sentensi hizi:
Kwa mfano:

a) Katarina atapewa kitabu kipya.





b) Mama atahudhuria lakini hatazungumza sana.



### Sentensi Changamano

Mbuzi aliyenunuliwa juzi amechinjwa leo asubuhi





## Uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia istilahi za kimuundo

Mkabala huu hutumika kuchanganulia sentensi kwa kuzingatia muundo wa vipashio vya sentensi. Kwa hiyo istilahi za kimuundo kama vile kirai nomino (KN), kirai kitenzi (KT), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE) na kirai kiunganishi (KU) ndizo hutumika katika uchanganuzi wa sentensi.


### Njia ya matawi

i) Mtoto Yule alikuwa anacheza mpira.



ii) Sentensi changamano

Kiti kilichovunjika kimetengenezwa




**Njia ya Jedwali**

i) *Sentensi* sahili

Maziwa ni lishe bora.

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | KT | | |
| N | t | KN | |
| | | N | KV |
| | | | V |
| Maziwa | ni | Lishe | bora |

ii) *Sentensi a*mbatano

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

| S – Ambatano | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| $S_1$ | | | | $S_2$ | | |
| KN | KT | | | KN | KT | |
| N | T | KE | U | W | T | KN |
| | | E | | | | N |
| Wanafunzi | wanafagia | darasani | na | wengine | wanapanga | viti |

## Tafakuri

Ndugu mwanafunzi, tunatarajia kwamba umefaidika vya kutosha kuhusu somo la ufafanuzi wa tungo. Umahiri huu uliopata utakuwezesha kuelewa dhana, dhima na aina za tungo na kuchanganua sentensi kwa kutumia njia ulizojifunza. Bila shaka somo umelipenda na kulifurahia. Iwapo umelipenda na kufurahia eleza kilicho kupendeza na kukufurahisha. Kama hukulifurahia utapaswa kueleza mambo yaliyo kutatiza na kutafuta ufumbuzi wake kwa wanafunzi wenzio na mwezeshaji.

## Zoezi la Nyumbani

Kwa kuwa umekamilisha somo la ufafanuzi wa tungo, ni matumaini yetu kwamba utakuwa umepata maarifa ya kutosha. Sasa jibu maswali yafuatayo:

1. Kwa kutumia mifano eleza kwa ufasaha maana ya:
   (i) Neno
   (ii) Kirai
   (iii) Kishazi
   (iv) Sentensi

2. Unafahamu nini juu ya:
   (i) Shamirisho
   (ii) Chagizo
   (iii) Kiima
   (iv) Kiarifu

3. Kwa kutumia mifano mbalimbali taja hatua za uchanganuzi wa sentensi.

4. (a) Soma kwa makini habari ifuatayo na ubainishe aina za sentensi zilizo katika habari hiyo.

   Kenge aliamka asubuhi sana na kuanza safari yake kwa miguu. Alifika kwenye pori lililo karibu na kijiji chao. Ghafla alisikia sauti nzito ya simba akiunguruma. Alikimbia sana na kujikwaa kwenye kisiki, mguu wake ukavunjika. Hivi sasa Kenge amelazwa hospitalini. Mguu uliovunjika umekatwa. Kama angeliwahi kufika hospitalini asingelikatwa mguu wake.

   (b) Changanua sentensi ambazo zimepigiwa mistari kwa njia ya matawi na jedwali.

## Faharasa

**Chagizo** — Kipashio cha kimuundo kama vile kielezi kinachojitokeza upande wa kiarifu ambacho huweza kudondoshwa na bado sentensi ikabakia na maana ya msingi.

**Mahakama** — Mahali ambapo kesi za mashitaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa.

**Msamiati** — Jumla ya maneno katika lugha fulani.

**Mnyambuliko** — Uzalishaji wa neno kutokana na kuweka viambishi kwenye kiini au mzizi au shina la neno.

**Ngeli** — Kundi la nomino katika baadhi ya lugha lenye sifa zinazofanana kisarufi.

**Ngoe** — Mchoro wenye umbo la mti usio na majani unaotumika katika elimu ya hesabu na isimu.

**Shamirisho** — Neno linaloashiria mtendwa au mtendewa au yambiwa katika sentensi.

**Tanakali sauti** — Unukuzi wa kitu kama vile sauti ilivyo.

**Tohoa** — Badilisha matamshi au tahajia ya neno la lugha ya kigeni ili lilinganena matamshi au tahajia ya lugha ya kienyeji. Kama vile 'shirt' (Kingereza) kuwa 'shati' (Kiswahili).

**Tungo** — Kipashio cha kimuundo kinachotokana na uwekaji pamoja wa vipashio sahili ili kujenga kipashio kikubwa zaidi.

**Upatanisho wa Kisarufi** — Utaratibu ambao kila nomino huwa inawakilishwa na mofimu katika maumbo mengine yanayohusiana nayo katika sentensi.

## Marejeleo


Maanga, G. & Mumbo, C. (2011). *Johari ya Kiswahili Kidato cha Tatu,* East African Education Publishers Ltd. Nairobi. Kampla, Dar es Salaam.

Mhilu, G. G. & Masebo, J. A. (2008). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kidato cha Tatu*, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mirikau, S. A. (2008). *Msururu wa PTE Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*, East African Education Publishers Ltd, Nairobi. Kampala, Dar es Salaam.

Njenge, S. (2011). *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Nne*, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita.* TET, Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. (2006). *Moduli ya Kumi Uhakiki wa Tamthiliya*, TEWW, Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (2006). *Moduli ya Tatu Fasihi kwa Ujumla,* TEWW, Dar es Salaam.

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la 3*. Oxford University Press, Dar es Salaam.

Alternative Secondary Education Pathway

Institute of Adult Education
P.O. Box 20679,
Dar es Salaam
Tel: +255 22 2150836
E-mail: info@iae.ac.tz,
Website: www.iae.ac.tz

ISBN 978-9976-88-168-4
9 789976 881684